AOC-275.2 Doc. Code: OEP
Rev. 6-23

www.kycourts.gov

KRS Sura ya 403;
KRS Sura ya 456;
FCRPP Sehemu ya IV

# AMRI YA ULINZI

❑ AMRI YA ULINZI WA DHARURA (EPO)
❑ AMRI YA MUDA MFUPI YA ULINZI WA MTU DHIDI MTU (TIPO)

Namba ya Kesi ____________

Mahakama

Wilaya ____________ Jimbo ____

Kitengo ____________

## MLALAMIKAJI/MDAI

____________

Jina la Kwanza Jina la Kati Jina la Mwisho

❑ Mlalamikaji anayewasilisha malalamiko kwa niaba yake mwenyewe; na/au

❑ Mlalamikaji anawasilisha malalamiko kwa niaba ya mtoto ambaye ametambulishwa humu.

**Watu Wanaolindwa na Amri hii:**

❑ Mlalamikaji: ____________ Tarehe ya Kuzaliwa: _______

❑ Mtoto ambaye Ombi limewasilishwa kwa niaba yake:

Jina: ____________ Tarehe ya Kuzaliwa: _______

❑ Mtu(watu) mwingine anayelindwa au mtoto(watoto) anayelindwa:

Jina: ____________ Tarehe ya Kuzaliwa: _______

Jina: ____________ Tarehe ya Kuzaliwa: _______

Jina: ____________ Tarehe ya Kuzaliwa: _______

Jina: ____________ Tarehe ya Kuzaliwa: _______

**Dhidi ya**

## MDAIWA/MSHTAKIWA

____________

Jina la Kwanza Jina la Kati Jina la Mwisho

Uhusiano na Mlalamikaji: ❑ mwenza ❑ mwenza wa zamani ❑ hawajaoana, wamezaa mtoto pamoja ❑ hawajaoana, wanaishi au waliwahi kuishi pamoja ❑ mzazi ❑ mtoto ❑ mzazi wa kambo ❑ babu/bibi ❑ mjukuu ❑ Kaka/Dada yangu aliye mtu mzima ❑ mtu ambaye anaishi kwenye kaya hiyohiyo kama mtoto au watoto iwapo mtoto au watoto wanadaiwa kuwa waathirika
❑ kwa sasa au hapo awali walikuwa kwenye mahusiano ya kimapenzi.
❑ hakuna uhusiano wowote kati ya uliotajwa hapo juu ambao ulikuwepo, lakini mdaiwa anatuhumiwa kwa kosa ❑ la kunyemelea au ❑ shambulio la kingono

Anwani ya Mstakiwa: ____________

____________.

## VITAMBULISHO VYA MSHTAKIWA/MDAIWA

| JINSIA | JAMII | Tarehe ya Kuzaliwa | Urefu | Uzito |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

| MACHO | NYWELE | Namba ya Hifadhi ya Jamii |
|---|---|---|
| | | |

| NAMBA YA LESENI YA UDEREVA | JIMBO | TAREHE YA MWISHO |
|---|---|---|
| | | |

Sifa Bainifu: ____________

____________

____________

____________

**TAHADHARI:** ☐ Silaha ilihusika ☐ Ana Silaha na ni Hatari ☐ Kesi ya Talaka/Malezi/Kumtembelea Mtoto inasubiri

**MAHAKAMA IMEBAINI:**

Kwamba ina mamlaka dhidi ya wahusika hao na jambo husika, na sheria ya Kentucky inampatia Mshtakiwa taarifa na nafasi ya kusikilizwa.

❑ Uamuzi wa ziada wa amri hii unaonyeshwa hapa chini.

**MAHAKAMA INAAMURU:**

❑ Kwamba Mshitakiwa azuiliwe kufanya makosa zaidi ya unyanyasaji au vitisho vya unyanyasaji, kunyemelea, au shambulizi la kingono

❑ Kwamba Mshitakiwa azuiliwe kufanya mawasiliano yoyote yasiyoruhusiwa na Mlalamikaji/Mdai au mtu yeyote anayelindwa aliyetajwa na Amri hii.

❑ Masharti ya nyongeza kwenye Amri hii ni kama inavyoonekana hapa chini.

Masharti ya Amri hii yataisha pale ambapo usikilizwaji wa shauri hili utahitimishwa kwa mujibu wa KRS 403.735 au KRS 456.050 isipokuwa kama utaendelea au utaondolewa kwa amri nyingine ya baadae ya mahakama.

**ANGALIA WITO WA MAHAKAMA ULIOAMBATANISHWA KWA AJILI YA TAREHE NA MUDA WA KUSIKILIZWA KRS 403.730; 456.040.**

*Mwendelezo wa wito wa EPO/TIPO ambao* ***haujapokelewa*** *una kikomo cha miezi sita. Iwapo Mdaiwa hajawahi kupewa amri hii na Mahakama bado haijaiondoa, amri hii itaisha baada ya miezi sita, tarehe* ____________, ______. KRS 403.735; 456.050.

**ONYO KWA MSHTAKIWA:**

**Amri hii itatekelezwa, hata bila usajili, wa mahakama za jimbo lolote, Wilaya ya Columbia, Himaya yoyote Ya Marekani, na inaweza kutekelezwa na Ardhi za Makabila (18 U.S.C. Kifungu cha 2265). Kuvuka jimbo, himaya, au mipaka ya makabila ili kukiuka amri hii kunaweza kusababisha kufungwa jela (18 U.S.C. Kifungu cha 2262).**

**Mahakama pekee ndiyo inaweza kubadilisha amri hii.**

FOR INFORMATIONAL PURPOSES ONLY NOT AN OFFICIAL COURT DOCUMENT
KWA AJILI YA TAARIFA TU SIO HATI RASMI YA MAHAKAMANI

Namba ya Kesi ______

**UMUZI ZIADA WA MAHAKAMA:** Baada ya kupitia ombi na kushauriana vya kutosha, mahakama imeamua kwamba madai yanaonyesha uwepo wa hatari kwa sasa ya ❑ukatili na unyanyasaji wa majumbani, ❑ukatili wa kimapenzi na unyanyasaji, ❑ unyemeleaji ❑ shambulizi la kingono.

**KWA HIYO, INAAMRIWA ZAIDI YA KWAMBA:**

❑ Mdaiwa azuiliwe kukutana au kufanya mawasiliano yoyote na Mlalamikaji na mtu/watu wengine wafuatao wanaolindwa: ______

❑ isipokuwa kama ifuatavyo: Mahakama inaona kuwa mawasiliano yafuatayo ni ya muhimu na yatafanyika kwa uchache, kwa hiyo yanaidhinishwa: ______

❑ Kwamba wakati wote na popote Mdaiwa atakuwa angalau umbali wa angalau futi ______ *(zisizozidi futi 500)* kutoka kwa Mlalamikaji na mtu/watu wengine wote wanaolindwa na Amri hii.

❑ isipokuwa kama ifuatavyo: Wahusika wanaruhusiwa kuwa katika sehemu zifuatazo za wazi wakiwa ndani ya umbali wa futi 500 katika mazingira yenye ukomo na vigezo maalum:

Eneo/anwani ya wazi: ______
Mazingira/Vigezo: ______
Eneo/anwani ya wazi: ______
Mazingira/Vigezo: ______
Eneo/anwani ya wazi: ______
Mazingira/Vigezo: ______

❑ Ya kwamba, baada ya Mlalamikaji kuonyesha hatari iliyopo, Mdaiwa azuiliwe kwenda au asiwe ndani ya umbali uliobainishwa wa maeneo yaliyobainishwa hapa chini:

Eneo: ______ ______ futi.
Eneo: ______ ______ futi.
Eneo: ______ ______ futi.

❑ isipokuwa kama ifuatavyo: ______

❑ Kwamba Mdaiwa azuiliwe kutupa au kuharibu mali zozote za wahusika.

❑ Kwamba Mdaiwa aondoke kutoka kwenye makazi yaliyokuwa yanatumiwa na wahusika kwa pamoja ambayo yapo (*taja anwani*) ______

❑ Kwa mujibu wa vigezo vya KRS 403.270, 403.320 na 403.822 , malezi ya muda kwa ______ yatolewe kwa ______

❑ Kwamba umiliki wa wanyama wafuatao wa nyumbani wanaomilikiwa na wahusika kwa pamoja atapewa Mlalamikaji:

Mnyama wa nyumbani: (*jina*) ______ (*aina/uzao*) ______ (*rangi*) ______
Mnyama wa nyumbani: (*jina*) ______ (*aina/uzao*) ______ (*rangi*) ______
Mnyama wa nyumbani: (*jina*) ______ (*aina/uzao*) ______ (*rangi*) ______

❑ *(chagua moja)*❑ Mlalamikaji au ❑ Mdaiwa ataruhusiwa kuchukua vitu vyake kutoka kwenye makazi ambayo wahusika wanayoishi pamoja ambayo yapo (*taja anwani*) ______ na vyombo vya usalama vinaagizwa kusaidia.

❑ Ili kusaidia kuondoa uwezekano wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa majumbani, ukatili wa kimapenzi na unyanyasaji, unyemeleaji, au shambulizi la kingono katika siku za usoni ______

*(Mahakama haiwezi kumuamuru Mlalamikaji kuchukua hatua thabiti. KRS 403.740; KRS 456.060)*

**UKIUKWAJI WA AMRI HII UTACHUKULIWA KUWA NI DHARAU KWA MAHAKAMA NA KUNAWEZA KUSABABISHA KUFUNGULIWA KESI YA JINAI. AFISA YEYOTE WA USALAMA ATAMKAMATA MDAIWA BILA HATI YA KUKAMATA IWAPO KUNA SABABU INAYOONYESHA KUWA UKIUKWAJI WA AMRI HII UMETOKEA. NI MAHAKAMA PEKEE YENYE UWEZO WA KUBADILISHA AMRI HII. MLALAMIKAJI AU MDAIWA ANAWEZA KUTOA HOJA YA KUREKEBISHA AMRI HII.**

| Tarehe Iliyotolewa | Hakimu |
|---|---|

Nakala kwa:
Faili la Mahakama; Mlalamikaji, Karani wa Mahakama kwenye Wilaya ambayo ni makazi ya kawaida ya Mlalamikaji, kama tofauti; Vyombo vya Usalama/kituo cha utumaji wa barua, waraka kinachowajibika kwa maingizo ya LINK; Vyombo vya Usalama vilivyoteuliwa kwa huduma; Idara za Huduma za Ndani ya Jamii (CHFS)

**Hakikisha taarifa za kwenye visanduku zimekamilika na zinasomeka.** Bila taarifa sahihi kwenye kila kisanduku, Amri **HAIWEZI** kuingizwa kwenye mfumo wa LINK.

Chapisha Fomu    Tengeneza Upya Fomu

FOR INFORMATIONAL PURPOSES ONLY. NOT AN OFFICIAL COURT DOCUMENT.
KWA AJILI YA TAARIFA TU. SIO HATI RASMI YA MAHAKAMANI.